**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI**
**KIZIDUO CHA KIKAO CHA MENEJIMENTI YA WAKUU WA IDARA NA VITENGO CHA MWEZI NOVEMBA, 2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI TAREHE 22/11/2021.**

**A). WATAALAM AMBAO WALIHUDHURIA**

1. Bw. George D. Haule -Mkurugenzi Mtendaji -Mwenyekiti
2. Bw. Mulsary A. Lukindo -Mkuu wa idara ya Ardhi na Maliasili -Katibu
3. Bi. Bertha M. Faustine -Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika
4. Bw. Ramadhani Ibrahimu -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
5. Dr. Zawagholi Charles -Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
6. Bi. Asha M. Ally -Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
7. Bi. Mwanaidi G. Herman -Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
8. Bi. Glory R. Mushi -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
9. Bw. Enock Mmari -Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
10. Bw. John J. Urassa -Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha
11. Bw. Simon Mwaiteleke -Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
12. Bw. John J. Mmbaga -Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
13. Bw. Paschal Masatu -Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji
14. Eng. Olais Simon Sikoi -Mkuu wa Idara ya Ujenzi
15. Bw. Hatibu B. Shekulwavu -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
16. Bw. Jackob C. Beatus -Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira
17. Bw. Ally F. Mtengo -Mwandishi wa kikao

**B). WATAALAM AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA.**

1. Bw. Kelvin Hosea Lefi -Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
2. Bw. Halid Salum Mkwizu -Afisa Biashara

**MUHT.NA. 41/04/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwasihi kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa kikao hicho. Baada ya kusema hayo, alitamka kufungua kikao mnamo saa 03: 30 Asubuhi.

**MUHT.NA. 42/04/2021/2022 KUPITISHA AGENDA**

Agenda za kikao ziliwasilishwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kupitisha Ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 22/10/2021.
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 22/10/2021.



CamScanner

5. Taarifa ya mapato na matumizi ya Fedha za Halmashauri kwa mwezi Oktoba, 2021.
6. Taarifa ya Kesi za Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Oktoba, 2021.
7. Taarifa ya ujenzi wa kituo cha afya Milingano
8. Taarifa ya Mapendekezo ya kuanzisha geti la Ukaguzi wa mazao na mapato mengine
9. Taarifa ya Ujenzi wa madarasa kwa fedha zinazotokana na UVIKO-19.
10. Maandalizi ya kikao Kijacho cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
11. Mengineyo
12. Kufunga kikao

*Baada ya ajenda hizo kuwasilishwa Mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanaziafiki agenda zilizowasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa ambapo wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzipitisha agenda hizo ili ziweze kujadiliwa katika kikao hicho.*

**MUHT.NA. 49/04/2021/2022 TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA NA NYUMBA YA MTUMISHI KWA FEDHA ZINAZOTOKANA NA UVIKO -19.**

Iliwasilishwa taarifa kuhusiana na ujenzi wa madarasa hamsini na nne (54) katika shule mbalimbali za sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ambapo ilielezwa kuwa Halmashauri imepata fedha za UVIKO-19 kiasi cha Tshs.1,170,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 54 kwa shule za sekondari Tsh. 1,080,000,000 na ujenzi wa nyumba ya watumishi kwa gharama ya Tsh. 90,000,000. Ujenzi wa madarasa hayo utawezesha kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasa uliopo na kuwezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza watakaojiunga na masomo katika mwaka 2022 kupata vyumba vya madarasa na kuendelea na masomo bila shida.

Aidha, ilielezwa kuwa zimeundwa timu za uratibu wa ujenzi nyumba na madarasa hayo kutoka kwenye menejimenti ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa madarasa hayo unafanyika kwa haraka na kukamilika katika muda uliopangwa. Timu hizo zimepangwa kitarafa katika tarafa tatu za Soni, Bumbuli na Mgwashi ili kurahisisha shughuli ya ufuatiliaji, kila tarafa itaratibiwa na kundi lenye watu nane waliochanguliwa na kupitishwa na ofisi ya Mkurugenzi kwa ajili ya kufuatilia ujenzi huo na kuhakikisha madarasa yanakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora unaotakiwa.



CamScanner

Mchanganuo wa kina kuhusiana na timu za uratibu zilizoundwa kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi huo, mpango kazi wa ujenzi wa madarasa 54 na nyumba ya watumishi kwa kutumia fedha za UVIKO-19 pamoja na shule zilizopokea fedha hizo kwenye akaunti za shule uliainishwa kwenye taarifa iliyowasilishwa.

*Baada ya majadiliano ya kina ya wajumbe waliipokea na kupitisha taarifa hiyo ya ujenzi wa vyumba 54 vya madarasa na nyumba ya watumishi kwa ajili ya utekelezaji.*

**MUHT.NA.52/04/2021/2022 KUFUNGA KIKAO.**

Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikamilifu katika kikao hicho. Mwenyekiti alifunga kikao Saa 05:00 Asubuhi.

**UMETHIBITISHWA NA:-**

**PROTAS L. DIBOGO**
**Katibu**

**GEORGE D HAULE**
**Mwenyekiti**

22/11/2021
**Tarehe**



CamScanner